



Hamadi A. Seneda ama Madee alizaliwa mwaka 1980 jijini Dar. Alisomea mjini Tanga mji ulioko

pwani ta Tanzania. Wimbo wake wa kwanza kazi yake mola ulipokelewa kwa mikono miwili na kumfanya kupokea mialiko ya kutumbuiza sehemu mbbali mbali Tanzania nan chi za jirani za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Madee alitoa albamu yake ya kwanza kazi yake mola miaka michache iliyopita na alishirikishwa katika kazi za wanamuziki wenzake kama MB Dogg, katika nyimbo kama latifa na ina maana. Albamu yake ya kwanza ilifanya vizuri katika mauzo hasa ukanda wa pwani wa afrika mashariki akijizolea mashabiki wa kike na kiume.

Mwaka 2007 madee alitoa albamu yake ya pili iitwayo yote maisha ikimshirikisha prodyuza maarufu nchini p funk. Albam hiyo inafanya vyema kwenye soko.

{youtube}twrVXARmwkQ{youtube}

Madee anasema anawapenda sana nelson mandela, Julius nyerere na Joachim chisano ambao anawaona kama mashujaa wake wa mfano. Anasema kuwa ndoto yake ni kuwa mwanasiasa mashuhuri siku za baadae akifanya kazi kuleta maendeleo ya Tanzania na bara la Africa kwa ujumla.